

## Maswali

1. Kornelio alitoka kwa taifa gani?
2. Alikosa nini katika maisha yake?
3. Mungu alimwambia afanye nini?
4. Watumishi wake walienda wapi?
5. Petro aliona nini kwa maono?
6. Mbona Petro alikataa kula?
7. Mungu alikuwa anafundisha Petro nini?
8. Nani aligonga mlango wa Petro?
9. Petro alienda kuona nani?
10. Petro alimwambia juu ya nini?
11. Petro alimuuliza Kornelio afanye nini?

## Majibu

1. Mrumi
2. Hakujua Yesu
3. Alitumwa kwa Petro
4. Yafa
5. Shuka imejaa wanyama
6. Baadhi ya wanyama walikuwa wachafu
7. Mungu anaweza kufanya kila kitu safi. Hata Wayunani.
8. Watumishi wa Kornelio
9. Kornelio
10. Yesu Kristo
11. Abatizwe

# SHULE YA JUMAPILI YA CBM



## Awamu ya 1 Mwaka wa 1

# 48 Kornelio

## Marejeo

Matendo ya Mitume 10

## Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Mungu anaita watu waaminio katika jina Yesu

## Maneno maalum

1. Kaisaria + Warumi + Kornelio + Mungu wa Israeli + omba + kosa kitu kimoja.
2. Maono + malaika + Petro + Yafa + tuma watumishi.
3. Njaa + shuka kubwa + wanyama + ua + shida + safi pekee + kataa + sauti + Mungu alifanya safi.
4. Somo + Wayunani + gonga mlango + enda.
5. Safiri + kutumwa na Kornelio + Yesu Kristo + Roho Mtakatifu + batizwa + Wayunani wa kwanza.

**48.1** Hapo Pwani ya Israeli kuna pahali paitwapo Kaisaria. Wakati wa Yesu na hata baada ya miaka, Warumi walikuwa na maaskari wengi pale. Israeli ilitawaliwa na Warumi. Mmoja wa maaskari aliitwa Kornelio. Aliishi Kaisaria miaka mingi na akajifunza kuhusu Mungu wa Israeli. Aliomba Mungu kila siku lakini alikosa kitu kimoja kwa maisha yake. Hakujuua Yesu.

**48.2** Siku moja Mungu akamtumia Kornelio maono. Malaika alimkujia na kumwambia kwamba Mungu alikuwa amesikia maombi yake. Ilimlazimu atumanishe mtu amuite Petro aje amwambie vile anaweza kumfuraisha Mungu zaidi. Petro aliishi mbali kidoko kule pwani pahali panapoitwa Yafa. Kornelio alituma watumishi wake wawili wamtafute.

**48.3** Mungu alimtumia Petro maono pia. Maono yalimjia Petro wakati alikuwa na njaa. Haikuwa maono ya kawaida. Aliona shuka kubwa ikateremka kutoka Mbinguni imejaa wanyama. Kulikuwa na wanyama tofauti tofauti wengi na ndege. Petro aliaambiwa asimame aue mmoja na akule. Kwa petro hii ilikuwa shida.

Wayahudi kama Petro walitakiwa wakule wanyama waliokuwa safi kulingana na sheria za Musa. Wanyama waliokuwa kwa shuka hawakukuwa safi. Petro alisema hajawai kula wanyama wachafu. Kwa hivyo hataua na ale. Sauti ilimjia na kusema kwamba Mungu alikuwa amefanya wanyama wote safi.



Mara mbili tena aliambiwa aue na akule. Sauti ilimwambia, "Mungu akifanya kitu chochote safi ni safi."

**48.4** Mungu alikuwa akifundisha Petro somo. Wayahudi walifikiria kwamba kila mtu asiye Myahudi ni mchafu mbele ya Mungu. Hawa watu tunawaita Wayunani. Kornelio alikuwa Mrumi na kufuatana na sheria Petro hawezi kwenda kwa nyumba yake. Mungu alikuwa anafundisha Petro kwamba mataifa yote sasa ni wasafi na alitaka kila mtu ajue Yesu Kristo. Mara tu maono yalipomalizika, watumishi wa Kornelio walibisha mlango wa Petro. Alipofungulia wageni mlango, alifikiria juu ya maono. Mungu alimwambia, "Enda na hawa watu."

**48.5** Petro alienda Kaisaria. Alikutana na Kornelio na kumuuliza juu ya Yesu Kristo. Kornelio na jamii yake walimsikiliza Petro. Walipokuwa wakimsikiliza Petro, Mungu aliwariki na kuwatumia Roho Mtakatifu. Kwa hivyo Petro aliwauliza wabatizwe kwa maji. Kornelio pamoja na jamii yake walikuwa Wayunani wa kwanza kubatizwa katika jina la Yesu.

